**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA USHETU**

Namba za Simu
Mkuu wa Shule 0766 759 224
M/Mkuu wa Shule 0710 630 085
Matron 0764 615 416
Patron 0754 602 504

Shule ya Sekondari Dakama
S.L.P. 20
**USHETU**
04/05/2026

Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi……………………………………………….

S.L.P……………………………

………………………………….

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI DAKAMA ILIYOPO HALMASHAURI YA USHETU MKOANI SHINYANGA**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano shule ya sekondari Dakama mwaka wa masomo 2026/2027.Shule ya sekondari Dakama ipo mkoa wa Shinyanga,halmashauri ya wilaya ya Ushetu.

   Ukiwa unatoka mkoa wowote ule panda magari yanayokwenda Kahama.Usafiri kutoka Kahama Mjini kuja shuleni ni wa uhakika kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 11:00 jioni kwa Hiace na mabasi makubwa yapitayo shuleni Dakama kuelekea Iboja. Utashushwa shuleni kabisa (**DAKAMA SEKONDARI**). Nauli hahali ni Tshs 5,000/= kwa Hiace na Tshs 4,000/= kwa mabasi makubwa magari haya hupatikana kwenye kituo cha mabasi ya abiria kilichopo eneo liitwalo DODOMA maarufu kama stendi ya **DODOMA**. Magari yote yaendayo Ulowa, Makazi, Kashishi kupitia **IBOJA** yatakufikisha shuleni. Usipande magari yaendayo Bulungwa, Butibu au Idahina. Hakikisha unapanda magari yanayopitia Iboja kisha omba ushushwe shuleni Dakama kabla ya kufika Iboja. Usafiri wa pikipiki, bajaji upo japo ni ghali. **Muhula wa masomo utaanza kwa tarehe itakayotangazwa na OFISI YA WAZIRI MKUU - TAMISEMI.**

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia: -**

2.1 **SARE YA SHULE (DARASANI**)

**A. WASICHANA**

(i) Njoo na sketi mbili (2) ndefu za dark blue (**kitambaa kiwe esteem namba moja**) na zinazokaribia kisigino / kifundo cha mguu, mshono wa linda boksi, sketi fupi hazikubaliki. (**Rejea kiambatanisho C**) mwishoni mwa fomu hii. Mwanafunzi yeyote atakaye kuja na sketi tofauti na maelekezo yaliyotolewa sketi hiyo haitapokelewa.

(ii) Mashati mawili (2) meupe ya **HALUWA** ya mikopo mifupi / nusu kanzu nyeupe kwa waislamu.

(iii) Soksi nyeupe kuanzia jozi mbili (2) na ziwe fupi za kati.

(iv) Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika vya kufunga kwa gidamu (Kamba)

(v) Rangi ya hijabu au kikofia chake iwe nyeupe kwa atakaye tumia na izingatie maadili ya kidini (Ndefu) ya darasani.

(vi) Sweta rangi ya dark blue.

(vii) Hijabu nyeusi kwa ajili ya kushindia kwa atakayetumia na izingatie maadili ya kidini.

**B. WAVULANA**

(i) Njoo na suruali mbili (2) rangi ya dark blue (**kitambaa kiwe esteem namba moja**) suruali iwe na marinda mawili kila upande mbele na pia iwe imekunjwa chini (turn up) na yenye upana usiopungua inchi 16" chini,na iguse kiatu, suruali za chupa hazikubaliki (**Rejea kiambatanisho C**).

(ii) Soksi nyeusi kuanzia jozi mbili (2) na ziwe fupi za kati

(iii) Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunika na siyo buti wala ghorofa (High Heeled Shoes) vya kufunga kwa gidamu (Kamba)

(iv) Mashati meupe mawili (2) aina ya **HALUWA** mikono mifupi yanayotosha kuchomekea

(v) Sweta rangi ya dark blue

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

(i) Madaftari 10 QUIRE 4

(ii) Rimu Nne (4) za karatasi nyeupe (A4) aina ya Double A au A1(kwa mwaka)

(iii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (Orodha imeambatanishwa katika kiambatanisho D). Nunua vitabu kadri Uchumi utakavyo kuruhusu siyo lazima ununue vyote vilivyo andikwa kwenye orodha,

(iv) Dissecting Kit kwa mwanafunzi anaesoma Biology (PCB) na Laboratory coat kwa wanafunzi wa PCB na PCM.

(v) Boksi moja la examination gloves kwa wanafunzi wote wanaosoma Biology kwa ajili ya dissection

(vi) Scientific Calculator kwa tahasusi za PCM, PCB, HGK, HGL na HGLi

(vii) Ndoo moja (1) ya lita 20, mfagio mgumu mmoja na laini mmoja kwa kila mwanafunzi

(viii) Jembe na mpini wake kwa wanafunzi wa tahasusi za HGL na HGK

(ix) Squeezer moja kwa wanafunzi wa HKL

(x) Shoka na mpini wake kwa wanafunzi wa PCM

(xi) Panga moja kwa wanafunzi wa PCB

(xii) Mkasi mmoja mkubwa wa kukatia maua kwa wanafunzi wa HGLi

(xiii) Lita tano (5) ya dawa ya kusafishia vyoo kwa kila mwanafunzi

**(xiv) Kila mwanafunzi aje na hati ya matokeo (RESULTS SLIP) ya matokeo yake ya kidato cha nne**

### 2.3 Michango mbalimbali Shule za Bweni

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa Uendeshaji wa shule | 65,000/= |
| 2 | Tahadhari | 5,000/= |
| 3 | Nembo | 5,000/= |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000/= |
| | Jumla | 80,000/= |

Michango ilipwe Benki ya NMB: A/C NA. **30601100137**

Jina la Akaunti ya Michango: **DAKAMA SECONDARY SCHOOL**

## 3. Sheria na kanuni muhimu za shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na:

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule

(iii) Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (Preparation)

(iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa

(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(vi) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule

(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa

(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote

(ix) Kutunza mali za shule

(x) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa za binadamu bila idhini ya daktari; na

(xi) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

**MUHIMU**

Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi; Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa.Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu; Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule

### 3.2 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na :-

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu / walezi na jamii kwa ujumla

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule

(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule

(vii) Kufuga ndevu

(viii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya

(ix) Uvutaji wa sigara

(x) Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa

(xi) Kupata ujauzito au kutoa mimba

(xii) Kusababisha mimba

(xiii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi

(xiv) Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni

(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

(xvi) Kudharau Bendera ya Taifa

(xvii) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na

(xviii) Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi


**3.3 Viambatisho na Fomu Muhimu**

(i) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali (angalia kiambatanisho B)


(ii) Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

3.4 Tafadhali soma kwa makini maelekezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**KARIBU SANA KATIKA SHULE YA SEKONDARI DAKAMA**



**Mwl Cosmas John Chamoto**



**NB** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI / MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

Mkuu wa Shule 0766 759 224

M/Mkuu wa Shule 0710 630 085

Mwandamizi Taaluma 0759 193 052

Mwandamizi Malezi 0764 615 416 / 0686 449 610

**KIAMBATANISHO A**

**MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI**

| **NA** | **MAHITAJI** |
|---|---|
| 1 | Godoro la sponji futi $2\frac{1}{2} \times 6$ |
| 2 | Blanketi kwa ajili ya baridi |
| 3 | Sanduku la chuma |
| 4 | Ndoo moja kwa ajili ya usafi binafsi |
| 5 | Mashuka manne (4), mashuka mawili ya rangi ya pinki na mawili light blue |
| 6 | Taulo, chupi au boxer za kutosha |
| 7 | Sabuni za kutosha |
| 8 | Mafuta ya kupaka |
| 9 | Lesso |
| 10 | Ndala / sendo / open shoes |
| 11 | Kiwi na brashi |
| 12 | Mswaki na dawa ya meno |
| 13 | Kitana |
| 14 | Kikombe cha uji / chai cha nusu lita |
| 15 | Kijiko |
| 16 | Sahani na bakuli |
| 17 | Chandarua cha mstatiri na si duara (ring) rangi ya ligh blue kwa wavulana na wasichana rangi ya pinki |
| 18 | Daftari kubwa (Counter Books quire 4) na kalamu za kutosha |
| 19 | Sketi mbili (2) za kushindia rangi ya kijivu zinazovuka magoti, mshono wa linda boksi kwa wasichana (Rejea kiambatanisho A) |
| 20 | Suruali mbili (2) za kushindia rangi ya kijivu na moja yenye maridha mawili mbele, iwe na turn up na yenye upana usiopungua inchi 16", suruali chupa hazikubaliki (Rejea kiambatanisho A) |
| 21 | Tochi / kurunzi (Isiwe ya kuchaji kwa umeme |

| | |
|---|---|
| 22 | Track suit pea moja (rangi ya bluu bahari) |
| 23 | Kitenge doti moja (wasichana) |
| 24 | VIFAA VYA MICHEZO<br>-soksi jozi mbili rangi nyekundu kwa ajili ya michezo<br>-Viatu vya michezo<br>-Jessy ya Dotimundi yenye rangi ya njano kwa wanafunzi wote |
| 25 | Tshirt za shule (darasani & kushindia) zinapatikana kwenye duka la shule |
| 26 | Raba za kushindia rangi nyeupe kwa kila mwanafunzi na open shoes |

Tanbihi

1. Mwanafunzi aje na Bank Pay in Slip moja (michango) ambayo ina jina la mwekaji ambalo ni jina la mwanafunzi husika
2. Mwanafunzi asije na nguo za nyumbani na simu haziruhusiwi kabisa
3. Mahitaji ya vitu vidogo vidogo yatapatikana (yanauzwa) kwenye duka la shule
4. Fika mapema shuleni (kabla ya saa 12:00 jioni) ili uweze kupokelewa na kupewa huduma mara ufikapo
5. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa track suit anaporipoti shuleni na si vinginevyo
6. Mwanafunzi ahakikishe amepima afya yake na kujaziwa fomu iliyoambatanishwa na maelezo haya kwenye hospitali / kituo cha afya cha serikali na siyo binafsi
7. Ni vyema mwenye Bima ya Afya NHIF na zingine zinazokubalika waje nazo shuleni kwa ambao hawana bima za NHIF na wanazihitaji zinapatikana kwa 50,400 tu kwa mwaka.
8. Wanafunzi wa kike wanaruhusiwa kusuka kuanzia mistari mine (04) na isizidi mistari sita (06), kusuka siyo lazima.

**KIAMBATANISHO B**
**OWM – TAMISEMI**
**USHETU DISTRICT COUNCIL**
**DAKAMA SECONDARY SCHOOL**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A** Date ____________________

To the Medical Officer From ____________________

THE HEADMASTER
DAKAMA SECONDARY SCHOOL
USHETU

____________________
____________________
____________________

Name of student in full______________________________ please examine the above as to his / her physical and mental fitness for a full time study (two years course)
The examination should include:-

(i) (a) Eye – sight (b)Hearing (c) Speech (d) Limbs (e)Chest (f) Veneral Diseases (g) Epilepsy (h) Leprosy

(ii) Cirrhosis
(iii) Other diseases
(iv) Pregnancy (For ladies)

**PART B (To be completed by Government Medical Officer)**
I have examined the above-named person and consider that he / she is physically and mentally **FIT / UNFIT** for a full time of four years study / course.

(i) (a) Eye – sight_________________
(b) Hearing ___________________
(c) Speech____________________
(d) Chest_____________________
(e)Veneral Diseases___________
(f) Epilepsy___________________
(g) Neurosis___________________
(ii) (a) Neurosis_________________
(b) Cirrhosis_________________
(iii) Other serious diseases________
(iv) Pregnancy __________________

**PART C**
Doctor's General Remarks_____________________________________________________

Signature: ______________ Designation __________________Station_______________

## KIAMBATANISHO C (SARE)

| WASICHANA | WAVULANA |
|---|---|
|  |  |
|  |  |

**KIAMBATANISHO D**

**ORODHA YA VITABU KWA KILA SOMO**

**1. HISTORIA**

- ✓ Saleh Yassin (2010), Essentials in Advanced Level History One & History Two
- ✓ Zisti Kamili (2010) History Advanced Level History One & History Two
- ✓ Shibitali C.K (2012) Contemporary historical Events, Advanced Level History Two & History One

**2. JIOGRAFIA**

- ✓ David Waugh (2009) Integrated Approach Physical Geography
- ✓ Zist Kamili (2024) Physical Geography Alive for Advanced level
  TIE (2024) practical Geography form five and six
- ✓ TIE (2024) Physical Geography form five and six

**3. ENGLISH LANGUAGE**

- ✓ Advanced Level Literature (Nyambari Nyangwine (2012)
- ✓ Nicholous Asheli, Practical Approach, Literature (2012)
- ✓ Betrayal in the City, Francis Imbuga
- ✓ Selected Poems – TIE
- ✓ An enemy of the people – Henrik Ibsen
- ✓ A hand out for Advance, Paschal Salaw, need Level English One
- ✓ I will Marry when I want – Ngugi wa Thiong'o
- ✓ A man of the People – Chinua Achebe
- ✓ The Beautyful Ones Are Not Yet Born – A. Armah
- ✓ A season by Waiting – David Omowale
- ✓ Advanced Level Literature – Nicholous Asheli
- ✓ The Wonderful Surgeon and Other Poems by Charles Mloka

**4. BAIOLOJIA**

- ✓ TIE (2024) Biology for advanced secondary schools form 5 & 6

**5. KEMIA**

- ✓ TIE (2024, Organic chemistry for A-level Secondary Schools
- ✓ TIE (2024), Physical Chemistry for A – Level Secondary Schools form five & six
- ✓ TIE (2024) General Chemistry and inorganic chemistry for A-Level Secondary School form five & six

**6. FIZIKIA**

- ✓ TIE (2024) Physics for Advanced secondary schools form 5 & 6
- ✓ CHAND ONE and TWO

**7. ADVANCED MATHEMATICS**

- ✓ Sillen S.I (2014) Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools – FV, FVI (GDY Publications Company Ltd DSM
- ✓ Tranter C.J (2006) "Advanced Level Mathematics 4th edition, Hroder Murray, London NW 1 3BH
- ✓ Advanced Mathematics for Advanced Secondary Schools by Tellem Majigwa

**8. GENERAL STUDIES**

- ✓ J,K (1974) Ujamaa – Essays onsoualism, London Oxford University Pries
- ✓ Saluhaya M.C (2003) Advanced Level General Studies
- ✓ Nyambari N (2018) Advanced Level GS notes form 5 and 6 Nyambari Nyangwine Publishers DSM
- ✓ Mkapa B.W (2019), My life, My purpose: Mkuki na Nyota Publishers, DSM

**9. KISWAHILI**

(i) KISWAHILI 1

1. Nadharia ya lugha ya Kiswahili: Kidato cha Tano na Sita – Nyambari Nyangine na Masebo (2010)
2. Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyuo – Kihore, Y.M. na Masamba, D.P.B: TUKI (2003)
3. Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la pili: English – Swahili Dictionary – TUKI
4. Sarufi miundo ya Kiswahili (SAMIKISA) – Masamba, D.P.B.

(ii) FASIHI 4. Kamusi ya Kiswahili Sanifu

1. Nadharia ya Fasihi kidato cha Tano na Sita – Masebo - +Oxford University Press
2. Tahakiki Vitabu Teule Vya Fasihi Kidato cha 5 na 6 – Nyambari Nyangine na Masebo

**TAMTHILIA (WALAU VITABU VIWILI**

1. Mukwawa wa uhehe- M.Mulokozi
2. Shujaa milambo- Emmanuel Mbogo
3. Usaliti mjini-Francis Imbuga

**RIWAYA (WALAU VITABU VIWILI)**

1. Dunia uwanja wa fujo –E. Kezilahabi
2. Mirathi ya Hatari-C. G. Mung'ong'o
3. Wasifu wa siti Bint saad –Shaaban Robert
4. Ua la Faraja- w.E. Mkufya

**USHAIRI (WALAU VITABU VIWILI)**

1. Wosia wa baba –Mohamed Amanzy
2. Andamo Msafir safarini – Mohamed Ghassani
3. Fumbo linaloelea- Nyangwine
4. Malenga wa ziwa kuu-Wallahi bin Wallah

**10. LITERATURE IN ENGLISH F5 & 6**

**NOVEL**

(i) Arrow of God written by Chinua Achebe, East African Educational Publishers
(ii) A man of the people written by Chinua Achebe East African Educational Publishers
(iii) A Grain of wheat written by Ngugi wa Thiong'o East African Educational Publishers
(iv) Petals of Blood written by Ngugi wa Thiong'o East African Educational Publishers

(v) No longer at Ease written by Chinua Achebe East African Educational Publishers
(vi) Joy Comes in the morning written by Hopolang phororo, Mkuki na Nyota Publishers Ltd.
(vii) The Lion of Yola written by Severine Ndunguru, E & D vision Publishing

**PLAYS**

(i) Betrayal in the City Written by Francis Imbuga, East Africn Educational Publishers Ltd.
(ii) I will Marry when I want Written by Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Mirii East African Educational
(iii) Julius Caesar by William Shakespeare East Africn Educational
(iv) Man of Kafira by Fransis Imbuga East Africn Educational

**POETRY**

(i) Poets of Africa 7: Boundless Voices Poem from Kenya by Arthur I.Luvai, East African Educational Publishers Ltd.
(ii) The bleeding Heart and other Poems by Shilia Kaaya, FGD Tanzania Ltd